# STEPPING OUT

## Getting Involved in Missions

# Kujihusisha katika Umisheni

**Life Challenge Assistance**
**Na**
**Hamasa ya Milele**

STEPPING OUT – Getting Involved in Missions

# Kujitokeza:
# Katika Umisheni

na

Reinhold Straehler

Hili ni Toleo la
**LIFE CHALLENGE**

Mei 2009 / Februari 2020

Box 50770–00200
Nairobi/Kenya
**www.life-challenge.org**

# Kujitokeza:
# Kujihusisha katika Umisheni.

> “Kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi!” Yohana 20:21

Hakuna ajuaye umri wa Sheikh Ibrahimu. Lakini ni wazi ana umri wa juu. Hata hivyo Sheikh Ibrahim huku akitabasamu kwa furaha, bado ana nguvu na hutembea kilometa chache kwenda kwenye kanisa ndogo kwenye milima kila Jumapili. Alikuwa mtu wa kwanza kubatizwa kati ya watu wa umri wa miaka 50 na zaidi akiwa angali kijana mdogo lakini mkakamafu wa kuelewa ulimwengu uliomzunguka.
Wakati huo kuna wageni waliotembelela mji wao, wageni hao walikuwa na ngozi ya rangi tofauti na waliongea lugha tofauti ya nchi ya mbali sana wakiwa na ujumbe mpya. Ulikuwa ujumbe wa Mungu anayewapenda wanadamu wote bila kujali lugha, rangi ya ngozi wala tamaduni. Ujumbe uliomguza sana Ibrahim akiwa mdogo na ukampa hisia kubwa za kutaka kuwa na uhusiani wa kibinafsi na huyu Mungu. Hivyo alichukua hatua ya kijasiri na akawa mfuasi wa kwanza wa Yesu Kristo katika jamii yake nchini Sudan. Kwa kuwa wafuasi wengine wa Yesu Kristo kutoka nchi ya mbali walikuwa wametumwa na makanisa yao, katika eneo hili la Sudan, walitatazika sana kufahamu maeneo ya kijiografia, na hata vizingiti vya lugha kwani iliwabidi wakabalieni na maisha katika mazingira mapya, walianzisha katika mpya. Kwa kuwa Ibrahimu alikuwa amechukua hatua ya kwanza, wengi waliomfuta. Siku hizikuna kanisa thabiti katika watu wa kikundi hiki.

Kisa hiki cha kweli kiliwezekana kupitia juhudi mwafaka kati ya Wakristo iitwayo “Misheni”. Tutachunguza kwa kindani ili tufahamu misheni hii ni nini hasa na jinsi inavyotuhusu sisi siku hizi.

## 1. Misheni: Nia ya Mungu

Kwanza tunahitaji kufafanua kitu kimoja muhimu sana. Misheni si jambo la uzunguni na chanzo chake si wanadamu. Badala yake mizizi yake imo katika asilia ya Mungu, Mungu anayetuma na anayeokoa*. Kujali huku kwa Mungu, kunapatikana kote katika Biblia*. Baada ya kuanguka kwenye dhambi kwa wanadamu wa kwanza, Mungu alikuja kuwatafuta Adamu na Hawa, akiwaita, "Uko wapi?" (Mwanzo 3:9). Hii inaonesha asili ya Mungu vizazi vyote. Mungu alikutafuta wewe na mimi! Mungu anawajali kwa watu wote!

Tuna mfano mzuri sana wa nia ya Mungu alipowakomboa wana wa Israeli kutoka Misri. Katika kitabu cha Kutoka 3:7-10 tunasoma jinsi Mungu alivyomuita Musa katika huduma hii mpya:

> *"Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri, nami nimekisikia kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao: maana nayajua maumivu yao; nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema, kasha pana; nchi ijaayo maziwa na asali."*

Hebu tafakari maelezo haya yaliyo dhahiri kabisa. Mungu anatazama kutoka mbinguni. Anaangalia kwa makini kabisa. Anaona mateso ya watu wake. Anaanza mpango wa kuwaokoa watu wake kwa kumtuma Musa kwa viongozi wa Misri. Mungu anawajali watu walio na mahitaji, amekusudia kuwasaidia. Kweli huyu ni Mungu wa ajabu!

Katika 1Timotheo 2:3-4 tunapata thibitisho kamili kwamba Mungu *"hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli*." Haya sio mapenzi ya mtawala mdhalimu, lakini mapenzi thabiti ya Mungu wa upendo. Hiki ndicho chanzo cha umisheni: katika asili ya Mungu na moyo wake wa huruma.

Tunataka tuhimizwe na nia hii. Tunataka tukuze mioyo inayotuchoma kwa ajili ya wale ambao bado hawajamjua huyu

Mungu wa upendo. Tunataka tuhusike katika misheni ya Mungu.

Kuna aina tofauti ya misheni ya Mungu:

a) Mungu ndiye chanzo cha umisheni. Ni mpango wake.
b) Yesu Kristo ndiye anayetekeleza misheni; kupitia kwa kufa na kufufuka kwake watu wanapatanishwa na Mungu.
c) Roho Mtakatifu anawezesha misheni.
d) Kanisa linatekeleza misheni.
e) Ulimwengu unapokea misheni. Kila mtu nafasi ya kusikia ujumbe wa Kikristo ya upatanisho.


Mukhtasari huu unatuonesha kwamba ingawa misheni ni nia ya Mungu, sisi kama kanisa tuna mchango mkubwa sana wa kuchangia. Kimsingi mani yetu ni ya umisheni. Hebu tuchunguze zaidi jukumu letu kama kanisa ni lipi.

## 2. Majukumu tofauti ya shughuli za kanisa

Kanisa la Sheikh Ibrahim kule Sudan, kama makanisa mengine, ni kanisa changamfu sana. Ingawa watu katika eneo hilo wamepitia wakati mgumu – wa vita, njaa, kuwa wakimbizi miongoni wa changamoto zingine – licha ya hao kanisa limehusika katika shughuli kadhaa muhimu; shughuli ambazo zimeelezwa kindani katika Neno la Mungu. Tunahitaji kuzingatia mambo manne muhimu ambayo kanisa la Sheikh Ibrahim linajihusisha nayo.
Shughuli hizi zinaweza kuonekana katika nyanja nne.

### 2.1 Ibada – Kutazama juu

Waumini wanapokusanyika katika kanisa la Sheikh Ibrahim, wao hupenda kumwabudu Mungu. Utatamani kuwasikia




wakiimba! Katika utamaduni wao kama Wasudan, nyimbo zilizotungwa na waimbaji wao wenyewe na wanamashahiri wao, wakitumia vyombo vinavyopendwa katika utamaduni wao, wanamsifu Mungu! Ibada yao inalenga kwa Bwana. Ni sifa na kumtukuza Mungu! (Tafadhali soma Zab. 95:6; Yn. 4:24; Efe. 5:19-20.)

Ni vema tu kuwa kanisa, ambalo mwenyewe ni Mungu, limsifu na kumtukuza. Katika shughuli hii, kanisa halijishughulishi na wao wenyewe na mahitaji yao, bali wanajishughulisha na jinsi Mungu alivyo. Lengo kuu la shughuli hii ni juu.

## 2.2 Kukuzana (kujengana ili kumfanya mwenzako awe na nguvu) – kutazama ndani


Kwa bahati nzuri, kanisa la Sheikh Ibrahim lina wazee wa Kanisa wa kutosha wanaoweza kufunza na kuelekeza watu katika Neno la Bwana. Wakati mwingine, mchungaji au mwinjilisti wa kanisa jirani anahubiri. Watu husikiza kwa makini ili waelewe Neno la Mungu. Ni furaha kuona jinsi Roho Mtakatifu anavyowapa vipawa vya kujenga mwili wa Kristo (Waefeso 4:11-13; 1 Wakorintho 14:12).



Baada ya ibada za kanisa watu huzungumza kwa muda mrefu, huku wakiwajulia wenzao hali. Katikati mwa wiki, wengi hutembeleana manyumbani na kuhimizana. Kukuzana hufanyika kupitia kwa mahubiri ambayo yanaendelea kanisani, na pia kupitia kwa ushirika kati ya washiriki. Lengo la shughuli ni ndani ya kanisa. Ni kama kujenga ukuta wa kuwakinga washiriki kanisani.

## 2.3 Uinjilisti – kutazama nje

Jambo moja katika kanisa la Sheikh Ibrahim ni kwamba hawakai tu ndani ya jengo la kanisa lao, bali wanatoka nje na kuwatembelea watu na jamii inayowazingira –hata wale ambao bado hawajaokoka. Wakulima katika mashamba yao, wanawake wanaouza mboga sokoni, wanaume wanaofanya kazi katika ofisi za serikali katika mji ulio karibu, washiriki wote kanisani wanawashirikisha watu wanaokutana nao upendo mkuu wa Mungu siku baada ya siku. Kulingana na maneno ya mwisho ya Yesu kwa wafuasi wake katika ili Amri Kuu, alichukulia uinjilisti kama sababu muhimu ya kuwa hai! (Tafadhali soma Mathayo 28:18-20; Yohana 20:21; Matendo 1:8.) *Wito wa kueneza Injii ni*



*amri.* Lakini mwito huu katika roho ya Mungu Baba, kutoka kwa upendo wake mkuu kwa watu wake waliopotea. Uinjilisti hufanywa kwa nguvu za Roho Mtakatifu na uwepo wa Yesu. Yesu haonekani, lakini yu pamoja nasi tunapozungumza kumhusu. Lengo la shughuli hii ni kutazama nje, kupita mipaka ya kanisa.

## 2.4 Kuhusika kijamii – Mtazamo wa nje sambamba

Licha ya amani ambayo imekuja katika eneo hilo, bado kuna mahitaji mengi katika jamii hiyo ambapo kanisa la Sheikh



Ibrahim lipo. Kadiri inavyowezekana, waumini wa kanisa husaidia kadiri wawezavyo. Wakati mwingine usaidizi huu unaweza kuwapikia chakula wazee katika jamii hiyo hasa wakati mkewe ni mgonjwa. Hivi karibuni kanisa lilisaidia kuchimba kisima ili kila mtu katika jamii – Wakristo and wasio Wakristo – waweze kupata maji safi.

*Kanisa haliko tu kwa ajili yake*. Kanisa halihusiki tu na maswala ya maisha ya milele ya watu. Kanisa lina jukumu la kutekeleza matendo ya upendo wa Kristo na huruma kwa Wakristo na wasio Wakristo. (Mathayo 5:13-16; 22:35-40.) Mfano wa kanisa la Sheikh Ibrahim ni Yesu Kristo aliyejali shida za maskini na wanaoteseka. Aliponya wagonjwa na hata mara nyingine kuwafufua wafu. Ikiwa kanisa linataka kuambatana na matakwa ya jamii, itahusika kwa kiwango fulani na huduma kwa wenye mahitaji na wanaoteseka. Lengo la shughuli hii ni kutazama nje ya mipaka ya kanisa.

Tumeona kuwa nyanja nne muhimu za ibada kanisani ni: kuabudu, kujengana kiroho, uinjilisti na kushughulikia maswala ya kijamii. Kama vile meza thabiti huhitaji miguu minne, vivyo hivyo shughuli hizi zinaleta uthabiti kanisani.

Kadiri mtu anavyopendelea kulifahamu kanisa la Sheikh Ibrahim ndivyo, utagundua kwamba kanisa hilo lina uthabiti wa mambo haya manne. Wanajua kwamba wakitaka kukua kiroho kama kanisa, sharti wawe waangalifu wasipuuze hata moja ya


nyanja hizi nne za maisha ya kanisa. Ingawa makanisa mengi yanajihusisha na kuabdu na kukuzana, mara nyingi nyanja ya uinjilisti na kuwashughulikia wasiojiweza haijakuzwa. Kwa hivyo tunahitaji kuangazia kwa makini huduma hizi mbili. Zote zinahusu kutoka nje ya mipaka ya kanisa. Hili huenda likawa si jambo la starehe kwetu, lakini halina budi kufanywa.

## 3. Kutoka nje ya mipaka ya kanisa

Katika Matendo 1:8 Yesu aliwapa wafuasi wake maelezo na ahadi kuhusu jukumu alilotaka watekelezeJe. *"You will be my witnesses in Jerusalem, in Judea, in Samaria and to the ends of the earth."* Hatua hizi tofauti za Amri Kuu za kuletea watu Habari Njema ya Yesu Kristo kwa ulimwengu zinaguzia mbinu tofauti za uinjilisti. Tofauti tu ilioko inatokana na tofauti za kitamaduni kati ya Mkristo anayeshuhudia Injili na ule mtu au watu ambao anawaletea Injili.

- **Uinjilisti "katika Yerusalemu" na "katikaYudea"**: Hii hufanyika katika maeneno ambapo Kanisa lipo, kati ya watu wa utamaduni sawa na pia lugha sawa.
- **Uinjilisti "katika Samaria"**: Hii hufanyika pale Wakristo wanapowashirikisha Injili na majirani wao, kwa mfano: watu wa kabila jirani ambao lugha na tamaduni zao zinakaribiana. Mara nyingi huwa na ushindani kati ya makundi haya mawili, hata hivyo hili ni jambo ambalo tunaweza kukabiliana nalo.
- **Uinjilisti "hadi mwisho wa dunia"** Hii inalenga kushiriki Injili na watu wa lugha na tamaduni tofauti. Ili kufanikisha jambo hili, Wakristo wanahitaji kujifunza lugha nyingine na kuiga tamaduni mpya, ili wawe shahidi kamilifu.

Mchoro ufuatao unaonesha hatua hizi katika uinjilisti:



Ili kufikia makundi haya yote, ni muhimu kwa Wakristo watoke nje ya mipaka ya makanisa yao. Washiriki wa kanisa la Sheikh Ibrahim wana furaha wakiwa pamoja kama washiriki. Lakini pia wanatazama nje ya jamii yao na kuwajali wale ambao bado hawajamjua Bwana Yesu Kristo. Hawangoji hadi watu hawa waje kanisani. Wao wanaenda pale walipo, katika soko, na hata pahali pao pa kazi.

Tunamsifu Mungu kwa yale yote Mungu amekuwa akifanya nchini Sudan. Jinsi makanisa yamenawiri miaka ya hivi karibuni. Mamia ya maelfu ya watu wamempokea Kristo. Tunakubali kwamba haya yote yamefanyika licha ya mateso, vita na unyanyasaji. Lakini licha ya vizingiti hivi kanisa limeendelea kukua. Hii ni sababu ya kuwa na moyo wa kushukuru na kumsifu Mungu.

Wakati huo huo tunahitaji tujue kwamba ukuaji huu mkubwa wa Kanisa uko tu katika sehemu fulani na katika tamaduni fulani ama makabila fulani. Sehemu zingine na jamii zingine hayajaguzwa hata kidogo. Kuna makabila mengi ambayo hayana kanisa. Bado kuna sehemu ambazo hamna Wakristo kabisa, na wakiwepo, ni wachacne mno.

Kanisa la Sheikh Ibrahim lina fahamu jambo hili. Linawahuzunisha sana. Dhehebu lao limetafakari sana na kuomba ni nini wanaweza kufanya dhidi ya jambo hili. Wanafahamu kwamba, kama *kanisa wanahitaji kujitokeza nje ya mipaka yao ya utamaduni na lugha.* Wanahitaji watoke “Yerusalemu” na “Yudea” na waende “Samaria”. Hadi ‘mwisho wa nchi’! Kwa hivyo, kama dhehebu nzima, walianza kupanga mipango halisi za kufanya kazi kati ya baadhi ya makabila hayo ambayo bado hayakuwa na kanisa. Waliwafunza wake na mabwana zao na kuwatuma katika maeneo tofauti, na kuwawezesha kwa kila njia. Hawa sasa ni mashahidi waishio kwenye maeneo ambayo hakuna Wakristo wengine. Wanashiriki Injili ya ajabu ya Yesu Kristo na watu ambao hawakupata nafasi hapo awali a kuisikia Injili ya Yesu Kristo. Wakristo wengi wanahitaji kufanya juhudi kuvuka mipaka ya

lugha na tamaduni na kuwafikia wale ambao bado hawajafikiwa na Injili.

Kujitokeza nje ya mipaka ya Kanisa ni muhimu pia ili tuweze kuyajali maslahi ya watu ya kimwili na hata hisia zao. Kanisa linahitaji kujitwika majukumu fulani ya jamii inayotuzunguka, pamoja na changamoto zao. Hii ndiyo sababu Sheikh Ibrahim ameanzisha mradi wa kuchimba kisima na pia ndio sababu baadhi ya washiriki kibanafsi wasaidia katika maeneo yao, pale panapotokea hitaji.

Kujitokeza huku nje ya mipaka ya Kanisa inajihusisha kwa kiwango kikubwa "umisheni" amabao ulimguza sana Sheikh Ibrahim alipokuwa mdogo na kuyaweka maisha yake kwa njia iliyo sawa.
Sasa tunarudi kwa swala tulilouliza hapo awali. Huu msukumo wa umisheni unatuhusu kivipi siku hizi?

## 4. Kutuma jinsi Yesu alivyotumwa

Neno "Umisheni" linatoka kwa neno la Kilatini "missio" na maana yake ni "kutuma". Kote katika Biblia tunaona jinsi Mungu alivyo Mungu wa kutuma. Aliwatuma manabii wake, Mwanawe na Roho Mtakatifu wake. Kutuma kwa mwanawe ndio ilikuwa kilele cha misheni ya Mungu. Lakini misheni hii ingali inaendelea! Mwana, Yesu Kristo, anawatuma wafuasi wake, yaani kanisa lake kuendeleza misheni yake. *"Kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi!"* (Yohana 20:21.)

Kanisa limetumwa ulimwenguni ili liwe chumvi na mwanga, kama isemavyo Mathayo 5:13-16. Ili kutimiza mwito huu kanisa linahitaji kuwatuma watu kwa mahitaji kamili fulani. Kanisa limeitwa kuhudumu na kushiriki katika maeneo yake ya karibu, na pia linahitaji kutuma vikundi na watu binafsi waanzishe huduma ya kushiriki Injili kule ambako Injili haijahubiriwa. Punde tu ufahamu wa misheni unakuwa katika Kanisa, hilo Kanisa litafahamu jukumu lao kutuma watu waanze huduma mpya.

Ukuaji mkubwa wa Kanisa nchini Sudan umefanyika bila kupangwa. Tunamshukuru Mungu kwa yale yameweza kiufanikishwa. Sasa ili kuanzisha kanisa kwenye maeneo ambayo hayana Kanisa, unahitaji mipango ya makini na kutuma vikundi maalum inahitajika. Hili ni jambo la dharura. Kanisa la Sheikh Ibrahim liligundua jambo hili na wakaanza kutuma watu katika maeneo mengine. Hata hivyo waligundua pia kwamba huu ulikuwa mwanzo tu. Mengi yalihitajika kufanywa.

Makanisa mengine huanza kuuliza jinsi wanaweza kushiriki katika mchakato wa umisheni siku hizi. Makanisa mengi nchini Sudan yana mizizi yao kwa wamishonari waliotoka nchi zingine. Karne kadhaa zilizopita watu walikuja kwenye maeneo yao na Habari Njema. Hata pale ambapo hawa wafanya kazi wa awali hawakuwa na hekima na kufahamu utamaduni wa watu ambao walikuwa wakiwahudumia, bado huo ulikuwa mwanzo wa Kanisa la siku hizi huko. Lakini sasa makanisa yako kila mahali nchini Sudan na yanahitajika kujua majukumu yayo hayo na kutuma wamishonari kutoka kwa washirika wao. Wanahitaji kutuma wamishonari kwa maeneo yale ambayo hamna Wakristo.

## 5. Tunaweza kufanya nini?

Sisi kama Kanisa na Wakristo binafsi tunahitaji kuhamasishwa na Roho Mtakatifu. Tunahitaji mwito mpya unaotuchoma wa kueneza Ufalme wa Mungu katika taifa hili na kuleta Injili kwa wale ambao bado hawajaisikia.

*Shughuli zote umishonari sharti ianze kwa maombi. Kama kanisa tunaweza kuwaombea wale walio katika jamii yetu na ambao hawamjui Bwana Yesu Kristo. Tunaweza kuombea jamii ambazo hazina kanisa miongoni mwao na ambao pia hawana watu wa kuwashirikisha Injili.*

Makanisa au madhehebu yanaweza yakachukua watu wa kabila fulani au eneo fulani la kijiografia ambao wataliombea na

kutayarisha watu wanaoweza kuhudumu huko. Makanisa au madhehebu ya eneo hilo wanaweza kutuma vikundi vya waumini katika eneo fulani. Huenda ikawa wanafanya kazi ya kawaida ili kujikithi kimaisha, lakini wanaenda kwenye eneo na lengo maalum la kuanzisha kanisa.
Kadiri watu wa tamaduni na makabila mengine wanavyokuwa Wakristo, tunahitaji tuwe tayari kukubali njia zao za kudhihirisha imani yao ambayo huenda ikawa tofauti na zetu kulingana na tamaduni zao. Hao ni dada na ndugu zetu hata kama wanadhihirisha imani yao tofauti na sisi!

Kote barani Afrika, Kanisa linachukua majukumu kuhusu umisheni, kufanya upendo wa Bwana ujulikane kote duniani, kuwasaidia wenye mahitaji, kubadilisha jamii, na kuwashirikisha kuhusu wokovu mkuu upatikanao katika Yesu Kristo. Kanisa la Sheikh Ibrahim huenda likawa ndogo na halina uwezo mkubwa wa kifedha likilinganishwa na makanisa mengine, lakini limejotolea kutii amri ya Kristo: “Kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi”. Kile ambacho Yesu alichowaambia wanafunzi wake miaka 2000 bado ni amri yake kwetu sisi mpaka leo.

Sasa ndio wakati wa kujihusisha na Umisheni!

*Tafadhali wasiliana nasi kwa maelezo zaidi jinsi unavyoweza kuomba na sote tushikane mikoni ili kuwafikia wale ambao bado hawajasikia Injili.*

**Life Challenge**
Box 50770–00200
Nairobi/Kenya
info@lifechallenge.de
**0717 – 179 445**

**Hamasa ya Milele**
SCRIPTURE MISSION
Box 11795
Arusha
hymilele@gmail.com
+255.767.288.053
+255.784.288.053